

**MUHTASARI YA MALALAMISHI YA *SAVE LAMU* NA *KWASASI MVUNJENI*
SELF-HELP GROUP YANAYOWASILISHWA KWA MSHAURI/MPOKEA
MALALAMISHI WA *INTERNATIONAL FINANCE CORPORATION***

Malalamishi imeandikwa kwa niaba ya *Save Lamu* na *Kwasasi Mvunjeni Self-Help Group*. *Accountability Counsel* na *National Justice* wanasaidia malalamishi kama washauri.

Malalamishi inaeleza kwamba *Save Lamu* na *Kwasasi Mvunjeni Self-Help Group* kwa pamoja wana hofu kubwa kuhusu hatari za kiwanda cha makaa kwa afya ya jamii zao, riziki, usalama wa chakula, mazingira na turathi za kitamaduni zenye thamani. Pia inaeleza namna matatizo haya yanavyochochewa na kutokuwa na mshauriano na ushirikishaji wa maana wa wanajamii katika kuandaa mradi huu.

Malalamishi yanawasilishiwa ofisi ya Mshauri/Mpokea-Malalamishi (au CAO), ambayo ni ofisi ya Malalamishi ya *International Finance Corporation (IFC)* ya *World Bank Group*. Tunaamini kuwa *IFC* inachangia kiwanda cha makaa cha *Lamu* kupitia uwekezaji katika benki tatu za biashara, *Cooperative Bank of Kenya*, *Commercial Bank of Kenya* na *FirstRand Bank* (uhusiano huu ulijulikana mda mfupi baada ya malalamishi kuwasilishwa). Baada ya kupokea fedha za *IFC*, benki hizi zilitoa mchango wa fedha kwa kampuni zinazohusika na ujenzi wa kiwanda cha makaa.

Tunaamini uwekezaji huu umekiuka na unaendelea kukiuka sera zilizoundwa ili kulinda jamii na mazingira, pamoja na mfumo wa viwango wa *IFC* uitwao ‘*IFC Performance Standards*.’ Malalamishi inaomba Mshauri/Mpokea-Malalamishi (CAO) afanye uchunguzi huru ili kujua kama mradi wa kiwanda cha makaa umefikia viwango vya sera hizi – mchakato ujulikanao kama tathmini ya ridhaa. Malalamishi inpeana hitaji kwa *IFC* kuchukua hatua za haraka kuzuia wateja wake kushiriki katika mradi mbaya na kutathminimiradi yoyote mipya katika sekta ya kifedha kwa makini na kuepuka kuchangia zaidi.

Malalamishi ina sehemu nne muhimu na vijisehemu vingi vinavyoshughulikia masuala ya mazingira na jamii. Sehemu muhimu ni:

- I. Utangulizi kuhusu kiwanda cha makaa kinachokusudiwa kujengwa katika Kaunti ya Lamu**
- II. Muhtasari wa uhusiano baina ya *IFC* na kiwanda cha Lamu cha makaa**
- III. Ukiukaji, na uwekezano wa ukiukaji, wa sera na taratibu za *IFC***
- IV. Juhudi za kuwasilisha masuala haya kwa *Amu Power*, wawekezaji na mamlaka zingine**

Hapa chini ni muhtasari wa kila sehemu.

I. Utangulizi kuhusu kiwanda cha makaa kinachokusudiwa kujengwa katika Kaunti ya Lamu

Sehemu hii ya kwanza inaeleza kuhusu kiwanda cha makaa kinachokusudiwa kujengwa Lamu na kufafanua hali yake katika Kaunti ya Lamu na *LAPSSSET*. Lengo ni kuweka wazi hatari zilizomo katika ujenzi wa kiwanda cha makaa, pamoja na maendeleo mengine makubwa yanayokusudiwa – katika eneo hili lenye utajiri mwingi wa kitamaduni na mazingira. Hoja muhimu ni pamoja na zifuatazo:

Kaunti ya Lamu: Eneo jepesi kuathirika kijamii na kimazingira

Kaunti ya Lamu imetambulikana kimataifa kwa ajili ya utajiri wa sehemu za baharini na mazingira ya ardhi. Ina sehemu za baharini zilizolindwa, misitu na mbuga za wanyamapori, pamoja na misitu ya Boni, na Mbuga za Dodori na Kiunga. Lamu ina asilimia sabini (70%) ya

mikoko ya Kenya – ambayo ni rasilmali kubwa inayolinda dhidi ya mmomonyoko wa ardhi na mafuriko na uzalishaji wa aina mbali mbali za samaki.

Kiwanda kinachokusudiwa na kitakachochukua eneo la ekari 975 kiko bara ya Lamu, karibu sana na misitu muhimu aina ya mikandaa eneo la Pwani. Ardhi inatwaliwa kwa lazima kutoka kwa wakulima ambao, miaka mingi tangu ilipotangazwa kuwa watafurushwa, wameendelea kuwa na hofu kuhusu kiwango na aina ya fidia na makazi mapya watakapopewa. Angalau wakulima mia moja na tisa (109) na familia zao katika eneo la Kwasasi wamefurushwa na ujenzi wa barabara ya kufikia eneo la kiwanda bila mashauriano ama fidia.

Eneo hili la kiwanda ni takribani kilomita 20 kaskazini mwa Lamu Old Town. Lamu Old Town ni mji uliotambuliwa na UNESCO kama turathi ya kimataifa. Ni mji wa kale na makazi ya Waswahili yaliyohifadhiwa vyema katika ukanda wa Afrika Mashariki. Ni jamii ndogo ya uhafidhina na inajilinda kwa kuimarisha ujenzi wa jadi na hali zake za kipekee za kijamii, kitamaduni, na kidini.

Wakazi wengi wa Lamu wana hofu kubwa kuhusu athari za kiwanda cha makaa kinachokusudiwa kujengwa katika maeneo haya yenye rasilmali kubwa za kimazingira na kitamaduni na wamekuwa wakiipinga. Mradi huu unahatarisha Lamu kutokana na uchafuzi wa hewa, maji na ardhi, udhoofishaji wa rasilmali za baharini na uharibifu wa mazingira ya makazi muhimu. Ufurushwaji wa watu na kiuchumi na uharibifu wa mazingira utakuwa na athari mbaya kwa afya, riziki, usalama wa chakula, na turathi muhimu za kitamaduni. Athari zitapatikana katika eneo zima la Lamu.

Wakaazi wa lamu wanaelezea;

“Tuna huzuni kuwa thamani yoyote ya kimazingira iliyoko katika eneo hili itapotea kabisa. tunaogopa kuwa vumbi itapulizwa na upepo wa bahari na inaweza kutulia karibu na nyumba zetu, mashamba na baharini. Kuna uwezekano wa uchafuzi huu kuletwa na maji na kuchafua mashamba na maji yetu”

Maelezo kuhusu kiwanda cha makaa cha Lamu

Mnamo Septemba 2014, serikali iliipata Amu Power mkataba wa kujenga kiwanda cha makaa. Amu Power ni kampuni maalumu iliyoundwa na Gulf Energy, kampuni ya nishati ya Kenya, na Centum Investment, kampuni ya uwekezaji ya Kenya. Mnamo Mei 2018, kampuni hizi zilitangaza mkataba wa ushirikiano na kampuni ya Merekani ya General Electric (GE) ili GE itoe teknolojia yake kwa Amu Power kuwezesha ujenzi wa kiwanda cha makaa, na nafasi kwa kampuni ya GE kupata hamu sawa katika kampuni ya Amu Power.

Kwa mujibu wa taarifa ya ESIA ya Julai 2016, kiwanda cha makaa kitakuwa na vitengo vitatu vya nishati ya makaa. [Licha ya tangazo la GE la Mei 2018 kuwa itatoa teknolojia ya kisasa kwa ajili ya kiwanda cha makaa cha Lamu, hakuajawa na uchapishaji wa tathmini ya kiufundi]. Kiwanda hiki cha nishati kitatoa megatani 2.8 (mt) za makaa kila mwaka. Kitafanya kazi masaa 24 kwa siku, siku saba kwa kila juma.

Kiwanda kitatumia aina ya mfumo wa baridi wa “kuweka baridi mara moja”. Mfumo huu utatoa maji kutoka Manda. Baada ya maji kupitia mfumo wa baridi, yatarudishwa Manda, huku yametolewa chumvi na yakiwa na joto.

Kiwanda kitatoa gesi ya moshi hewani kufikia mita 210 kwenda juu. Maji ya bahari yatatumiwa kuosha gesi ya dohani. Jivu lithafadhiwa katika eneo la jivu kavu.

Kiwanda cha makaa pia kitahitaji mfumo ufuatao:

- Uchimbaji wa chokaa katika eneo la Witu. Kibali cha uchimbaji wa ekari 2,000 tayari kimetolewa na mamlaka ya kaunti. Chokaa inahitajika ili kudhibiti mfumo wa uchafuzi uitwao ‘utoaji salfa kwenye gesi majimaji ya dohani’ Chokaa hii itasafirishwa kwa njia ya barabara na bahari kwenda kwa kiwanda cha nishati;
- Mfumo wa kupokea makaa pamoja na buntwa katika bandari ya Lamu, vifaa vya kupokea makaa na mfumo wa takribani kilomita 15 wa kuhawilisha makaa kutoka bandarini hadi zizini la muda;
- Mazizi mawili ya makaa, yanayoweza kuhifadhi metriki tani 420,000 za makaa;
- Kistesheni cha kv 400;
- Eneo la wafanyakazi linaloweza kukaliwa na watu baina 250 hadi 300;
- Mfumo mpya wa gari moshi ya kusafirisha makaa endapo makaa ya Kenya yatapatikana; na
- Barabara, majengo na mifumo mingine kwa ajili ya kazi hii.

Ijapokuwa uandaaji wa barabara ya eneo – na ufurushwaji wa wakulima wa Kwasasi – unaendelea, ujenzi wa kiwanda cha makaa bado haujaanza. Angalau wakulima 109 na familia zao wamepoteza mapato na usalama wa chakula, bila fidia au mashauriano.

LAPSSET

Ulewaji wa kiwanda cha makaa cha Lamu kinachokusudiwa na athari zake utawezekana tu kupitia ufahamu wa hali ya mradi wa LAPSSET. Lamu ni kitovu muhimu cha miradi ya LAPSSET pamoja na bandari yenye magesho ya meli 32, vifaa vya kiwanda, mifereji ya mafuta, mji wa kitalii, uwanja wa ndege, kiwanda cha kutoa chumvi na nyanya za umeme, ambavyo vyote viko katika hali tofauti za ujenzi.

Serikali ya Kenya inaeleza kiwanda cha makaa cha Lamu ni mradi ‘shirikishi’ wa LAPSSET. Hata hivyo, uhusiano baina ya miradi hii unaonekana kuwa wa karibu sana. Pamoja na uhusiano mwingine, mamlaka ya LAPSSET (LAPPSET Development Authority) ndiyo inayotwaa ardhi kwa ajili ya kujenga kiwanda cha makaa.

Kuna mgawanyiko katika Jamii ya Lamu kuhusu kiwanda cha makaa, pamoja na miradi mingine ya LAPSSET. Kama ilivyoelezwa katika Sehemu ya III ya Malalamishi, wanajamii wengi wana hofu kuhusu athari za kiwanda cha makaa na wameshiriki katika maandamano ya kukipinga. hasa hii ni kweli pindi watu wanapopata habari kuhusu athari zinazoweza kutokea kwa sababu ya mradi huu. Hata hivyo, baadhi ya wanajamii wamejitokeza kuunga mkono ujenzi wa kiwanda hiki kutokana na ahadi za ajira, fidia na maendeleo ya kiuchumi. Hofu hizi na mgawanyiko huu huchochewa na ukosefu wa mashauriano ya kina na wanajamii walioathirika.

II. Muhtasari wa uhusiano baina ya IFC na kiwanda cha Lamu cha makaa

Ni vigumu kufuatilia fedha za ujenzi wa kiwanda cha Lamu kwa sababu hakuna uwazi. Hata hivyo, kutokana na taarifa chache zilizoko, tunaamini kuwa IFC inachangia ujenzi wa kiwanda cha Lamu kupitia wateja watatu, Kenya Commercial Bank, Cooperative Bank of Kenya na FirstRand Bank (uhusiano huu wa tatu ulijulikana mda mfupi baada ya malalamishi kuwasilishwa na ukaelezewa kwa kina katika barua ya ziada iliyowasilishwa kwa CAO). Baada ya kupokea fedha za IFC, benki hizi zilitoa msaada wa kifedha kwa kampuni zinazohusika na ujenzi wa kiwanda cha makaa cha Lamu.

Miradi muhimu ya IFC, kwa ajili ya malalamishi haya, ni ifuatayo

Mradi wa IFC	Aina ya msaada wa fedha	Tarehe ya kuidhinishwa	Hali
Kenya Commercial Bank			
Kenya Commercial Bank – Mradi 32805	Mkopo	Mei 16, 2013	Hai
Kenya Commercial Bank – Mradi 36791	Mkopo/labda hisa bila riba	Septemba 22, 2016	Hai
Co-Operative Bank of Kenya			
Coop Bank of Kenya –Mradi 31321	Mkopo	Oktoba 5, 2012	Hai
Coop Bank of Kenya II –mradi 35393	Mkopo	Disemba 22, 2015	Hai
Coop Bank of Kenya III –Mradi 41133	Mkopo	Mechi 27, 2018	Hai
AMSME Coop Bank – Mradi 601493	Huduma ya ushauri	Oktoba 11, 2016	Hai
DFS Coop Bank Phase 2 – Mradi 602467	Huduma ya ushauri	Oktoba 12, 2017	Hai
FirstRand Bank *haikuwekwa wazi katika tovuto rasmi ya miradi ya IFC*			
Kampuni ya usimamizi wa mali ya IFC ilitoa dola za Marekani million mia moja sabini na mbili nukta tano (US\$ 172.5 million) kwa aina ya deni ya chini kwa FirstRand Bank	Mkopo wa kubadilika (moja kwa moja kubadilika kuwa hisa bila riba)	Aprili 2014	Hai

Katika hali zote hizi, IFC inatoa msaada wa fedha au ushauri kwa benki za Kenya ili kuzisaidia kutoa mikopo. Japo baadhi ya miradi hii inataja biashara ndogo na za wastani (SME) kama sekta muhimu inayoungwa mkono na IFC, hakuna ushahidi kuwa fedha za IFC ni mahsusi (zimekingwa) ili kusaidia sekta hiyo tu. Badala yake, tunaamini fedha hizo za IFC ziko katika benki za Kenya kusaidia shughuli zingine za fedha.

Baada ya kupokea fedha kutoka kwa IFC, Cooperative Bank of Kenya, Kenya Commercial Bank na FirstRand Bank zimesaidia kampuni zinazohusika na kiwanda cha makaa cha Lamu:

- Mnamo 2014 Cooperative Bank of Kenya ilitoa hati ya ukopeshaji ya Dola za Kimarekani US\$ milioni 5 kwa ajili ya pendekezo la Amu Power la kujenga kiwanda. Hati ya ukopeshaji huu inaonekana kuwa bado iko hai, ni bima kwa manufaa ya Kenya Power & Lighting Company ambayo ina mkataba wa miaka 25 wa kununua umeme kutoka kwa kiwanda cha makaa cha Lamu – endapo Amu Power itashindwa kukifanyisha kazi kiwanda hiki kufikia tarehe za maafikiano.
- Pamoja na hayo, Cooperative Bank ina uhusiano ulio hai na wa muda mrefu na Centum Investments. Hivi majuzi mnamo April 3, 2017, Cooperative Bank ilitoa Shilingi Milioni 981.5 kama deni la ovadrafti linalopewa uhai kila mwaka.

- Commercial Bank of Kenya imeipa Centum Investments mkopo (takribani bilioni 1.2) ambao kampuni hii inaweza kuchukua kadri inavohitajika ili kugharimia mahitaji yake ya biashara (pamoja na fedha za kiwanda cha makaa cha Lamu).
- Mnamo Septemba 2017 FirstRand Bank ilitoa mkopo wa ushirika wa milioni hamsini dola za Marekani kwa kampuni ya Centum Investment itakayokomaa mwaka wa 2021 (imeelezwa kwa kina katika barua ya ziada iliyowasilishwa tarehe 3 Mei 2019).

Msaada wa kifedha unaotolewa kwa Centum unawakilisha msaada mkubwa wa fedha kwa ajili ya kiwanda cha makaa cha Lamu. Centum ni mwanahisa mkubwa (51%) wa Amu Power. Mkurugenzi Mkuu wa Centum (James Mworio) anaonekana kushiriki sana katika mipango ya kiwanda cha makaa cha Lamu.

Hii sio mara yetu ya kwanza ya kutambua uhusiano baina ya IFC na kiwanda cha makaa cha Lamu. Wateja wengine wawili wa IFC – Equity Bank Limited na Standard Bank of South Africa – wanaonekana kutafuta fedha kwa ajili ya kiwanda cha makaa cha Lamu hao mwanzoni. Inawezekana pia uko uhusiano mwingine tusiojua baina ya IFC na kiwanda cha makaa cha Lamu.

III. Ukiukaji, na uwekezano wa ukiukaji, wa sera na taratibu za IFC

Uwekezaji wa IFC katika Kenya Commercial Bank, Cooperative Bank of Kenya na FirstRand Bank unatawaliwa na viwango vya utendakazi uitwayo ‘2012 IFC Performance Standards’ (IFS PS na sera ya IFC kuhusu mazingira na uendelevu wa jamii uitwao ‘IFC Policy on Environment and Social Sustainability (IFC Sustainability Policy’), pamoja na sera zingine zinazohusika. Sera hizi kwa pamoja zinawajibisha IFC na wateja wake kuchukua hatua kuepuka, kukinga na kudhibiti hatari za kimazingira na kijamii zinazoweza kutokana na kiwanda cha makaa cha Lamu. Licha ya kwamba mradi huu ndio unaanza, ukiukaji mkubwa wa sera hizo umeanza kudhihirika.

Sehemu hii ya Rasimu ya Malalamishi ina takribani kurasa 53 zinazofafanua hofu za jamii kuhusu athari za kimazingira na kijamii kwa undani. Hapo chini mna vijishemu na hoja muhimu kwa muhtasari:

A. Kenya Commercial Bank na Cooperative Bank hazifuati viwango vya IFC PS na IFC haisimamii majukumu haya

Sehemu hii inawasilisha hoja kwamba udhaifu wa tathmini na mashauri ya Amu Power ni mkubwa hivi kwamba ni wazi kuwa benki za Kenya Commercial Bank, na Cooperative Bank na IFC zimeshindwa kufuatilia na kusimamia hatari za kimazingira na kijamii zinazoweza kusababishwa na wateja wake. Hoja hizi pia zinagusia FirstRand Bank, ambayo uhusiano wake na IFC na kiwanda cha makaa baada ya malalamishi kuwasilishwa.

IFC PS 1 inaagiza kwamba IFC ifuatilie tathmini za hatari za kimazingira na kijamii zinazoweza kusababishwa na wateja wake ili kuhakikisha kuwa hatari hizo zinabainika na mipango ya kuziondoa ipo. Kuhusu uwekezaji wa IFC katika benki nyingine, kama vile Kenya Commercial Bank, Cooperative Bank of Kenya na FirstRand Bank, IFC inapaswa kufuatilia shughuli zote za benki hizo ili kutambua hatari zilizomo na kueleza hatua zinazotakiwa kuchukuliwa ili kuondoa hatari hizo. IFC pia inapaswa kufuatilia na kusimamia mara kwa mara uwekezaji wake ili kuhakikisha kuwa benki hizi zinafuata kanuni za IFS PS.

Sera za IFC PS1 na IFS Sustainability Policy pia zinaagiza Kenya Commercial Bank na Cooperative Bank kufanya tathmini zake za hatari za kimazingira na kijamii kuhusu uwekezaji wake kwa Centum Investments na Amu Power.

Hakuna taarifa iliyotolewa kwa umma na IFCama wateja wake kuonyesha kuwa zinachukua hatua maalumu kutekeleza maagizo ya IFC PS. Kama tunavyoeleza hapa chini benki hizi zinafanya kinyume chake na kukiuka viwango vilivyowekwa. Tuna hofu kuwa, kadri mradi utakavyoendelea, ndivyo ukiukaji huu utakavyokuwa mkubwa zaidi.

B. Tathmini ya kimazingira na kijamii haina sehemu muhimu za mradi

Tathmini ya kina ya athari za kimazingira na kijamii iliyotolewa kufikia sasa ni ile ya Julai 10, 2016 (2016 ESIA) iliyoandaliwa na Kurrent Technologies kwa ajili ya Amu Power. Lakini ripoti hii haijakamilika kamwe.

Pamoja na udhaifu mwingine, haijatathmini athari muhimu za vipengee na vifaa vingine vya mradi kama vile:

- Uchimbaji makaa na usafirishaji pamoja na mfumo wa kuhawilisha wa kilomita 15;
- Uchimbaji wa chokaa katika eneo la Witu; na
- Barabara ya kufikia kiwanda ya kilomita 9 ambayo imewaondoa angalau wakulima 109 na familia zao kutoka makao yao bila fidia au mashauriano.

Pamoja na hayo, kwa muda wa takribani miaka miwili tangu Ripoti ya ESIA kuchapishwa, Centum, Amu Power na GE, zilitangaza kuwa GE itatoa teknolojia ya kisasa (USC), ambayo ni ya kiwango cha juu ikilinganishwa na teknolojia ya SC inayotajwa na Ripoti ya ESIA ya 2016, kwa ajili ya kiwanda cha makaa. Lakini bado kampuni hizi hazijafanya tathmini ya athari inayozingatia teknolojia hii mpya ya GE.

Udhaifu huu unatilia shaka malengo ya IFC PS na mchakato wa ESIA. Wateja wa IFC hawana budi kufanya tathmini kamili na za kina kuhusu hatari za kimazingira na kijamii zinazoweza kusababishwa na mradi unaokusudiwa. Wanapaswa pia kuchukua hatua za kupunguza na kuzuia hatari hizo. Kutokamilika kwa Ripoti ya ESIA ya 2016 kumeathiri mchakato wa mashauriano, kwa sababu upeo wake haukuwa na vipengee muhimu.

C. Mashauriano wanajamii ni ya juujuu na hayajakamilika

Kanuni nyingine muhimu sana ya IFC PS ni mashauriano ya maana na yenye kina na jamii yenye ufahamu. Kwa sababu kiwanda cha makaa cha Lamu kitahusu “athari kubwa kwa jamii inayoathiriwa” sera ya IFC PS inaagiza kuwe na mchakato wa Ushiriki na Mashauriano yenye Ufahamu (ICP).

- Ushiriki huu unahitaji ubadilishanaji wa taarifa na ujumuishaji wa maoni ya jamii inayoathirika katika mchakato wa kutoa maamuzi.
- Mchakato wa mashauriano unapaswa kutilia maanani maoni ya wanawake na wanaume, na ubainishe matatizo na vipaumbele tofauti vya wanawake na wanaume;
- Mchakato uhifadhiwa katika maandishi, hasa hatua zilizochukuliwa ili kuepuka au kupunguza athari kwa wanajamii, na jamii zilizoathirika zifahamishwe namna matatizo yao yanavyoshughulikiwa.

Watu Asilia Walioathirika sharti washirikishwe kwenye mashauriano na, katika hali maalum, Miradi ihtaji Kibali Huru, cha Kabla, na chenye Ufahamu (FPIC) wao: Tazama Sehemu F hapo chini.

Mashauriano hadi sasa hayajafikia viwango hivi.

Mikutano kuhusu huu mradi ilifanyika mapema mwaka wa 2015 lakini ikasitishwa ghafla mnamo Juni 2015. Wakati huo, hakukuwa na habari za kina ama za maana kuhusu mradi huu, athari zinazoweza kutokea (pamoja na athari kubwa za kijamii zinazohusu afya, hewa na

uchafuzi wa maji, kuhifadhi jivu na uhamishwaji na upataji wa makazi mapya) au hatua zilizopendekezwa za upunguzaji makali ya athari. Brosha ya mradi zilizowasilishwa katika mikutano kadhaa haikuwa ya kina na iligusia kwa juu athari mbaya, haikutafsiriwa kwa lugha ya wenyeji, Kiswahili, na ilikosa kushughulikia vipengele muhimu vya mradi. Katika mikutano mingine, washiriki hawakupata vifaa vyovyote vya mradi.

Sera ya ESIA ya 2016 ina maelezo ya ziada kuhusu mradi. Hata hivyo, inashindwa kujibu kwa kikweli maoni na matatizo yoyote yaliyotajwa katika mikutano ya kijamii ya hapo awali. Kwa mfano, licha ya wasiwasi uliotolewa na wanajamii kuhusu eneo litakalotumiwa kwa ajili ya mradi huo, kutokuwepo kwa utathmini wa mifumo mbadala, mfumo wa baridi, uchafuzi wa hewa, uwanja wa jivu na taka nyingine hatari, mradi kama ulivyobuniwa wa ESIA umefanana sana na maelezo ya mradi yaliyotolewa katika mikutano ya hapo awali. Sera ya ESIA haijatoa maelezo kwa nini ilishindwa kushughulikia matatizo mazito ya wanajamii.

Tunafahamu kuhusu mkutano mmoja wa jamii uliofanyika baada ya ESIA kuchapishwa. Mkutano huu uliofanyika Agosti 26, 2016, hauwezi kuchukuliwa kuwa mashauriano kwa sababu, baada ya kubadilisha eneo la mktano katika dakika ya mwisho ulifanyika mahali ambapo hapakuweza kufikiwa na wakazi wengi wa Lamu kutokana na umbali wa kusafiri na gharama. Wanachama wa Kwasasi Mvunjeni Farmers Self-Help Group hawakuwa na habari ya kwamba mkutano huo unafanyika; hawakujilishwa wala kuambiwa na kwa wakati huo hawakuwa na habari ya kwamba wataathiriwa na barabara inayokwenda kwa eneo la mradi.

Maoni ya umma kuhusu ESIA na uidhinishaji wa serikali ni thibitisho kuwa ushirikiano wa wadau haukutuliwa maanani. Licha ya hitilafu nyingi zilizotajwa katika maoni ya umma yaliyowasilishiwa Mamlaka ya Taifa ya Mazingira ya Kenya (NEMA), shirika hilo liliidhinisha leseni ya ESIA mnamo Septemba 7, 2016, siku sita tu baada ya kufungwa kwa kipindi cha utoaji maoni ya umma. Idhini hiyo haikuhitaji mabadiliko yoyote kwa ESIA kwa mujibu wa maoni ya wadau.

Fauka ya hayo, wadau wa mradi waliotambuliwa na ESIA hawajumuishi makundi yote yatakayoathiriwa na mradi huo. Kwa mfano, kama ilivyo elezwa hapo awali, wakuliwa walio adhiriwa na barabara ya kupita hawakushauriwa. Zaidi ya hayo, orodha ya wadau wa mradi haikujumuisha wakazi wa Witu, hata ingawa ESIA ya 2016 inathibitisha kuwa kibali cha utwaji wa ardhi katika eneo la Witu kilitolewa mahususi kwa lengo la uchimbaji wa chokaa. Vile vile, jamii asilia zilizoathirika na kiwanda cha makaa zimetengwa.

Mwisho, tabia ya kutishwa na viongozi wa serikali imekwamisha majaribio ya vikundi vya mtaa kuendesha vikao vya kutoa habari ili kujadili na wanajamii athari za mradi. Maafisa wa serikali mara kwa mara wametoa vikwazo ili kuzuia mikutano ya kijamii kufanyika na hata kuonyesha madharau kwa juhudi za asasi za kiraia. Save Lamu imekumbwa na vitisho vikubwa kwa njia ya uchunguzi wa jinai ambazo zimeisha baada ya vamizi la uchunguzi. Wanaharakati wengine wa Lamu pia wamekumbwa na vitisho. Ripoti ya hivi karibuni ya Human Rights Watch na Kenya National Coalition of Human Rights Defenders imenakili unyanyaswaji na kutishwa kwa angalau wanaharakati wa mazingira 35 waliopo Lamu na polisi, wanajeshi na viongozi wengine was Serikali kati ya miaka ya 2013-2018, ikiwemo wanaharakati wanaopinga kiwanda cha makaa cha Lamu.

D. Nyaraka za mradi hazijachambua na kuonyesha hatua za kupunguza makali ya uchafuzi wa hewa na maji, uanuwai wa viumbe, mfumo wa mazingira na athari za hali ya anga

Sera ya IFC PS 1 inawajibisha uchukuaji wa hatua ili kuepuka, kupunguza na kufidia athari za kimazingira na za kijamii. Pia, Sera ya IFC PS 3 (ya umakinifu wa rasilimali na kuzuia

uchafuzi), PS 4 (Afya ya jamii na usalama) na PS 6 (Uanuwai wa viumbe, uhifadhi na usimamizi endelevu wa rasilimali za asili zenye uhai) zimeweka maagizo maalum ya kuepuka na kupunguza kuharibiwa kwa mazingira ya asili, pamoja na athari zinazohusiana na afya ya jamii na riziki. Pamoja na majukumu mengine muhimu, kuna yafuatayo:

- IFC PS 3 imeagiza kuwa miradi itumie mbinu bora za kuzuia uchafuzi wa mazingira ili kuepuka au, ikiwa kuepuka hakuwezekani, kupunguza athari mbaya kwa afya ya binadamu na mazingira;
- IFC PS 4 vile vile imeshurutisha kwamba miradi iwe na hatua za kukinga ambazo zinalingana na mazoea mazuri ya viwanda kimataifa ili kuepuka au kupunguza kabisa athari kwa afya ya jamii na kuhakikisha usalama; na
- IFC PS 6 inahitaji, kama jambo la kipaumbele, miradi iepuke athari kwa viumbe na mfumo wa mazingira (manufaa ambayo watu wanapata kutokana kwa mazingira). Majukumu yanapewa nguvu zaidi wakati mazingira ya kiasili na makazi muhimu yanapohusika.

Mipango ya kiwanda cha makaa cha Lamu haitimizi majukumu haya kwa njia kadhaa.

1. *Data ya kimsingi haitoshi*

Hatua ya kwanza ya kutambua hatari za kijamii na kimazingira ni ukusanyaji wa “data ya kimsingi ya hivi karibuni ya kimazingira na kijamii katika kiwango sahihi cha maelezo” (IFC PS 1.) Tathmini ya athari za kimazingira iliyojumuishwa kwa 2016 ESIA iitwayo ‘Ecological Impact Assessment Study’ haijafikia kiwango hiki.

Kwa mfano, maelezo ya sehemu ya kwamba utafiti wa ndege uliangazia eneo moja kwenye sehemu moja kwa masaa machache tu, wakati wa siku ambapo ndege hawako katika shughuli zake za kawaida. Upungufu huu na mapungufu mengine, yamefanya iwe vigumu kuamini matokeo ya utafiti.

Utafiti wa mamalia (wanyama) vile vile unaeleza kwamba sampuli zilikuwa na upungufu wa siku tano pekee kwenye eneo na matokeo yake yakawa kuna wanyama waliolengwa ambao hawakusampuliwa kabisa. Haikuwezekana kufanya sampuli wakati wa usiku na wakati wa masika kwa sababu ya wasiwasi wa usalama (kuzuia ziara za usiku) na vikwazo vya wakati.

Utafiti wa maeneo ya baharini ya mvua ya maji na maji safi na viumbe vya baharini pia ulikuwa na vikwazo. ESIA ya 2016 inakiri kwamba jitihada za uchukuaji wa sampuli za wanyama wa baharini wasio na na uti wa mgongo, nyasi za majini, uvuvi, miamba ya matumbawe na mikoko zilikuwa “chini ... kwa sababu siku za kuchukua sampuli zilikuwa kumi pekee.”

Mapengo haya katika kukusanya maelezo ya eneo zimeharibu sana matokeo ya msingi.

2. *Tathmini ya athari za uanuwai wa viumbe haina habari muhimu.*

Kama ilivyotajwa hapo juu, IFC PS 6 inajumuisha mahitaji magumu ili kuepuka athari kwa uanuwai wa viumbe na huduma za mazingira.

Katika Kaunti ya Lamu mna viumbe kadhaa vya baharini vinavyolindwa na sheria, msitu na hifadhi ya wanyamapori ambazo zinastahili ulinzi wa ziada kama makazi asili na muhimu chini ya IFC PS 6. Hasa;

- Kaskazini mashariki mwa eneo la mradi kuna Mazingira ya Msitu wa Boni-Lungi, pamoja na Boni na hifadhi za kitaifa la Dondori. Hifadhi hizi kwa pamoja zinaunda sehemu ya ardhi ya mapokeo ya Waaweer (Boni).

- Pia kaskazini mashariki mwa eneo la mradi, Hifadhi la Kitaifa ya Kiunga (Kiunga Marine National Reserve) inajumuisha pwani na visiwa 50 na miamba ya matumbawe katika eneo la Lamu. Eneo hili limeteuliwa kama sehemu ya UNESCO Biosphere.
- Kusini magharibi mwa eneo la mradi, karibu na mahali panapokusudiwa kuwa na machimbo ya chokaa, mna hifadhi ya msitu wa Witu inayojulikana kuwa na angalau aina tisa za mimea iliyotishiwa, pamoja na *Euphorbia tanaensis* iliyohatarishwa sana.

Tunahofia kuwa kiwanda cha makaa cha Lamu kinaweza kuhatarisha eneo hili na sehemu zingine muhimu kimazingira. Hata hivyo, 2016 ESIA haitjatoa maelezo kamili ili kupima kikamilifu athari hizo. Kwa hivyo pia inashindwa kutambua hatua za kutosha za kuepuka na kupunguza makali ya kiwanda. Kwa mfano;

- Athari za uzoaji*: ESIA 2016 inakiri kuwa shughuli za uzoaji wakati wa ujenzi zinaweza kusababisha uharibifu mkubwa kwa makazi jirani ya mikoko, nyasi za baharini na miamba ya matumbawe. Hata hivyo, inakosa kutoa makadirio ya uharibifu wa eneo-hasa na athari za uvuvi. Kwa mfano, ESIA haijakadiria kiasi cha vifaa vitakavyozolewa au kutathmini uwezekano wa athari za mchanga. Hatua za kupunguza makali (kama vile kuweka mipaka kwa wakati na njia za uzoaji) hazijatiliwa mkazo kabisa.
- Kutega viumbe vya baharini katika mfumo ya kuingiza maji ya baridi*: Licha ya kuweco kwa teknolojia isiyoathiri sana, kiwanda cha makaa kinapendekeza kutumia mfumo wa baridi ya mara moja. 2016 ESIA inakiri kuwa viumbe vya baharini vinaweza kuathiriwa na mfumo ya kuingiza maji na/au skrini ya nje ya valvu ya kuingiza baridi. Hata hivyo, haijaoa tathmini yoyote ya kiwango cha athari (kwa mfano, ni viumbe vingapi vitaathiriwa na mabadiliko husika ya mazingira ya bahari). Wala haijapendekeza hatua zozote za kuepuka au kupunguza makali ya athari hizo.
- Athari kutoka na maji kupanda joto*: Mfumo wa baridi ya kupitia mara moja unaokusudiwa na mradi huu utatoa maji ya baridi iliyotumika na kuirudisha katika kisiwa cha Manda na joto ya 9 digrii Celsius zaidi ya joto ya maji iliyoko. ESIA ya 2016 inakiri kuwa uchafuzi kupitia joto hili unaweza kudhuru viumbe vya baharini na viumbe uhai. Hata hivyo, ESIA ya 2016 haichambui eneo-hasa ili kueleza kiasi cha athari, ambayo inaweza kuwa janga kubwa sana.
- Athari kutoka kwa eneo la jivu*: Kulingana na ESIA ya 2016, taka ya majivu kutoka katika kiwanda cha makaa itawekwa katika eneo la majivu lenye uwezo wa kuhifadhiwa kwa miaka 15. Hakuna mikakati yoyote ya kurejesha taka kama inavyohitajika na IFC PS 3. Maeneo za majivu yanahitaji kiasi kikubwa cha ardhi na ina hatari kubwa za kimazingira na afya ya jamii pamoja na kuvuja na uchafuzi wa hewa. ESIA inaeleza kwamba eneo hilo huwa na monsuni zinazoweza kueneza na kuharibu majivu. Licha ya hayo, haijatoa haijaleza jinsi jivu litakavyohifadhiwa baada ya miaka 15 inayokadiriwa- licha ya muda wa mradi kuwa miaka 25- au jinsi taka hiyo itakavyofanyiwa baada ya kufungwa kwa kiwanda. Mwisho, ESIA ya 2016 haijaleza jinsi itakavyodhibiti hewa itakakayotoka kwenye hifadhi la jivu – jambo ambalo imejadiliwa zaidi katika sehemu ya uchafuzii wa hewa hapo chini.

Katika kutamatisha, ESIA ya 2016 haijazingatia athari kwa uanuwai wa viumbe katika mfumo wa kichukuzi cha makaa cha kilomita 15 kinachopangwa na pia uchimbaji wa chokaa katika eneo la Witu.

Bila habari hizi, mradi hauwezi kuchukua hatua mwafaka za kuepuka na kupunguza makali ya athari mbaya, wala kujua kwa usahihi thamani ya huduma za uanuwai wa viumbe na mazingira yatakayoharibiwa.

3. *Uharibifu wa huduma za mazingira*

Pamoja na viwango vya kulinda mazingira, IFC PS 6 inatilia mkazo ulinzi maalum kwa huduma za kimazingira. Huduma za kimazingira ni faida ambazo watu wanazipata kutokana na mazingira, kama vile bidhaa au huduma zinazounga mkono usalama wa chakula, riziki au utamaduni. Kiwanda cha makaa kinachopendekezwa kitaleta hatari kubwa kwa huduma za kimazingira zenye *kipaumbele* tukizingatia kuwa jamii nyingi za Lamu hupata riziki zake ilhali wengi wa jamii za Lamu bado hutegemea njia za kiasili kama vile uvuvi, kukata mikoko, uwindaji na kukusanya, ufugaji wa mifugo, kilimo, utalii wa kimazingira na mengine mengi ambayo yataathirika na kiwanda cha chokaa kinachopendekezwa. Wakaazi wa Lamu wanaelezea:

“Sisi wavuvi na wakataji wa mikoko tunatambua kwamba kukamilika kwa mfumo wa upoozeshaji wa Amu kutahatarisha Maisha ya viumbe wa majini. Hii ni kutokana na kiwango cha maji kupungua baada ya kunyonywa kutoka katika bahari na kupeleka kwenye mitambo na kurudishiwa tena baharini yakiwa maji ya moto. Mfumo huu wa upoozaji utaleta vifo Vya viumbe wengi wa majini ama madhara mengine kam kujeruhiwa kwa viumbe hao kutokana na kunasa katika mitambo hiyo.

Tunaelewa pia mfumo wa upoozaji utahatarisha misitu yetu ya mikoko kwani itaathiriwa na maji moto yenye kemikali kutoka kiwandani. Tunachukizwa kuona kwamba ikolojia itaathiriwa kwa kiasi kikubwa na kupeleka kupoteza rasilimali zetu ambazo ni muhimu kwa maisha yetu ya kila siku.”

“Sisi Wakulima katika kaunti ya Lamu Tunaelewa pia kuwa uchomaji makaa husababisha uchafudhi wa hewa ambao ni mchanganyiko wa kaboni na kemikali nyinginezo. Mchanganyiko huu unaweza Kuleta athari kama mzua yenye kemikali ambayo itaathiri mimea na maisha ya binadamu kwa ujumla. Tunaogopa kuwa madhara haya yataathiri ustawi wetu na pia afya zetu.”

“Rasilimali zetu ni vivutio vya watalii. Tuna watalii wanaokuja Lamu kushuhudia tamaduni za kiasili za kiswahili. Wanakuja Pia kufirahia fukwe zetu za bahari kuogelea na kusafiri katika mitubwi yetu.”

“Misitu ya mikoko ni muhimu katika ikolojia na uchumi wa Lamu kwa sio tu ni mazalia ya viumbe wengi wa majini lakini pia ni chanzo chá uchumi wa watu wetu.”

ESIA ya 2016 inakiri kuwa huduma kadhaa za mazingira zaweza kufutiliwa mbali au kupunguzwa na mradi. Hata hivyo, inashindwa kubainisha tathmini yoyote ya kina ya kiwango au wigo wa madhara hayo.

Fauka ya hayo, ESIA inabainisha hatua mbili tu zinazokusudiwa za kupunguza makali: (1) kuunga mkono ujenzi wa vyanzo mbadala vya riziki kwa wanajamii; na (2) kusaidia utekelezaji wa sheria za uvuvi ili kuzuia uvuvi zaidi au uvuvi katika maeneo yaliyolindwa. Hakuna maelezo zaidi yanayotolewa.

Hakuna hizi za kupunguza makali ya athari haziwezi kamwe kuhifadhi au kurejesha huduma za kimazingira kwa wanajamii. Badala yake, hatua zote mbili zinabainisha mkakati wa kumaliza au kupunguza tabia za jadi za uvuvi katika eneo la mradi. Jambo hili litasababisha kupoteza riziki na pia maarifa ya jadi na kwa hivyo turathi za kitamaduni. Mbajuni mmoja anaeleza kuwa upotezaji wa turathi za kitamaduni tayari umeanza: “Tulikuwa tunajua jinsi ya

kutengeneza dau vizuri, lakini ujuzi huo unapotea...” Upotevu wa turathi za kitamaduni utakuwa mbaya zaidi kwani wakazi wengi wanaondoshwa kwenye riziki za jadi.

Zaidi ya hayo, hatua zilizopendekezwa na ESIA zimekosa kabisa kushughulikia athari za maisha ya watu ambao sio wavuvi. Kwa hiyo uchambuzi huo haujakamilika kabisa.

4. Athari ya uchafuzi wa hewa hazijathminiwa vyema

Kama viwanda vyote vya makaa, kiwanda cha Lamu kitasababisha uchafu wa hewa ambao utaathiri afya na mazingira. Hasa, kiwanda hiki kitatoa dioksidi ya salfa (SO_2), oksidi za nitrojeni (NO_x), chembechembe hewani (PM), na zebaki. Licha ya madai kwamba jambo hili halitatokea, kiwanda cha makaa cha Lamu kitasababisha uzalishaji huo hata kama teknolojia yake itaboreshwa kutoka kwa kupewa teknolojia ya kisasa zaidi.

Kwa mujibu wa IFC PS 3, kiwanda cha makaa cha Lamu kinahitajika kutumia mbinu za kuzuia uchafuzi ambazo ni bora zaidi ili kuepuka athari za afya kwa binadamu na kwa mazingira Hata hivyo, kama ilivyojadiliwa hapo chini, tathmini ya uchafuzi wa hewa iliyomo katika ESIA 2016 inashindwa kufikia viwango vya IFC:

(a) *Tathmini wa msingi wa uchafuzi wa hewa haiaminiki*: Tathmini ya msingi ya ubora wa hewa ina udhaifu mkubwa na jambo hili linahatarisha tathmini zote zinazotegemea data hii. Ni vigumu kuamini baadhi ya matokeo ya msingi na wataalamu wamesema ‘hayawezekani kamwe.’ Kwa mfano, baada ya vipindi vifupi vya kupima, tathmini ya msingi imepata viwango chembechembe hewani zenye kipenyo cha chini cha au sawa na mikrometri 2.5 – $PM_{2.5}$) kwa kiasi kikubwa chini ya viwango ambavyo aghalabu hupatikana katika mazingira ya kawaida. Pia kuna tofauti kubwa katika matokeo yaliyoripotiwa katika eneo moja la ufuatiliaji katika sehemu tofauti za tathmini.

(b) *Ukosefu wa kutosha wa athari za uchafuzi wa hewa*:

Okside ya Nitrojeni (NO_x): Uzalishaji wa NO_x hauthiri afya, ikiwa ni pamoja na ugonjwa wa kupumua. Miongozo ya IFC juu ya viwanda vya nguvu za umeme hupendekeza kwamba kiwanda kipunguze uzalishaji wa NO_x kwa njia ya kuchomwa moto kwa kutimiza meko za chini za NO_x , kiwango cha chini cha kupiga hewa, na udhibiti wa NO_x kwa boila. Ingawa ESIA ya 2016 inasema kuwa kiwanda cha makaa cha Lamu kitatumia boila ya chini ya NO_x , haikutaja kama hatua yoyote ya ziada iliyopendekezwa na IFC itaingizwa katika awamu ya kuchora kiwanda.

Salfa Dioksidi (SO_2): SO_2 pia inahusishwa na athari za kupumua. Kulingana na ESIA ya 2016, kiwanda cha makaa cha Lamu kitapunguza uzalishaji wa SO_2 kwa kuanzisha mfumo wa maji ya bahari ya gesi ya dohani ili kuondoa salfa (FGD). Miongozo ya Mazingira, Afya na Usalama ya IFC inabainisha kwamba FGD za maji ya bahari, licha ya ufanisi wake, zina athari mbaya za asili katika mazingira ya baharini ambayo yanahitaji kuchunguzwa kwa makini. ESIA ya 2016 haizingati athari hizo za baharini

Chembechembe hewani (PM): $PM_{2.5}$ husababisha matatizo mbalimbali ya afya kwa wanadamu. ESIA ya 2016 inasema kuwa chombo cha kuondoa chembechembe hewani (ESPs) kitatumika ili kukamata PM kutokana na mafuriko, dohani na vishikamoshi bila kutaja teknolojia maalumu ambayo itatumika na jinsi itakavyokuwa. Zaidi ya hayo, ESIA ya 2016 haitaji athari za chembechembe za ziada (wakati NO_x na SO_2 zikichanganya na kemikali nyingine za hewa ili kuunda aina za $PM_{2.5}$), japo ni chanzo kikubwa cha $PM_{2.5}$ kutokana na viwanda vya makaa.

Zebaki: Zebaki inahusishwa na athari mbaya za afya kwa binadamu, ikiwa ni pamoja na athari za neva. Njia ya msingi ambayo wanadamu huwa na zebaki ni kwa kula samaki. Hii ni shida kubwa kwani uvuvi wa bahari ni shughuli ya pili kwa ukubwa katika uchumi wa Lamu. ESIA ya kiwanda cha Lamu inashindwa kutaja teknolojia yenye ufanisi ya kuchunga kwa kitambaa ili kupunguza kasi ya uzalishaji wa zebaki. Zaidi ya hayo, FGDs za maji ya bahari (aina ya mfumo wa kuondoa salfa uliopendekezwa kwa kiwanda wa Lamu) zimeonyesha ukweli kwamba kiwango cha juu cha zebaki kinazalishwa katika chimbuko lake. ESIA ya 2016 inashindwa kushughulikia athari hii.

Taka kutoka kwenye makaa na majivu: ESIA ya 2016 inashindwa kutathmini kiasi au athari zinazoweza kutokana na taka ya makaa na majivu ikielezea tu kwamba "hakuna taarifa ta kutosha wala data ya kuaminika" ili kujua athari kamili.

Mvua ya asidi: ESIA ya 2016 inakubali kuwa kiwanda cha nguvu za umeme cha Lamu kinaweza pia kuwa na madhara mabaya, yasiyokuwa ya moja kwa moja, kwenye mazingira kutokana na mvua ya asidi. Hata hivyo, haizingatii athari kwenye majengo laini ya chokaa na miamba katika mji wa Lamu, eneo ambalo ni Turathi za Kimataifa za UNESCO. Asidi inayeyesha vifaa hivi ikichanganyika na kemikali zingine.

Kwa sababu zote zilizotajwa hapo juu, uchambuzi wa athari za uchafuzi wa hewa katika ESIA hautoshi kukidhi majukumu magumu ya kupambana na uchafuzi yaliyowekwa na IFC PS 3, 4, na 6.

5. *Tathmini ya athari ya mabadiliko ya hali ya hewa*

IFC PS 3 pia inahitaji mteja kuzingatia njia mbadala na kutekeleza mbinu zinazoweza na za gharama ya chini zinazoweza kupunguza uzalishaji wa gesi (GHG) unaotoka kwa mradi, ili kupunguza athari za mabadiliko ya hali ya hewa.

Ripoti ya Mabadiliko ya hali ya hewa ya Mtaalamu wa GHG inasema kwamba kiwanda cha makaa cha Lamu ...kitaongeza uzalishaji wa GHG wa nchi kwa kati ya 6% -10%. Hii ni kinyume cha moja kwa moja na Mpango wa Kazi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa wa Kenya na ahadi za Kenya chini ya Mkataba wa Paris.

Licha ya hii, ripoti hiyo inashindwa kupima athari za mabadiliko ya tabinach kutokana na mradi ama ya vigezo vya nishati mbadala kwa kiwanda cha makaa cha Lamu.

E. Madhara ya kusambaza yamepuuzwa

Mbali na hatari kali za mazingira, maelfu ya watu wanaweza kuhamishwa kutokana na kiwanda hiki cha makaa. Kwa mujibu wa utafiti wetu wenyewe, tunaamini kwamba athari za makazi mapya kutoka kwa kiwanda cha makaa ya mawe cha Lamu ziko katika makundi manne, ikiwa ni pamoja na wanajamii asilia;

1. Uhamisho wa wakulima takribani 675 kutoka mashamba ambamo mna eneo ya mradi;
2. Uhamisho wa wawindaji, wakusanyaji, wafugaji wa nyuki na wavunaji wa mikoko na watumiaji wengine wa rasilimali kutoka kwenye eneo la mradi,
3. Uhamisho wa wakulima angalau 109 kutoka mashambani yalivyovukwa na na barabara ya kufikia eneo.

4. Ufurushwaji kiuchumi wa wavuvi na waendeshaji wa utalii kutokana na uharibifu wa mazingira, vikwazo vya usafiri wa meli na vikwazo vingine vikubwa kwa hali na ubora wa eneo la Lamu.

IFC PS 5 (kuhamishwa kwa lazima) inatumika katika sehemu zote za madhara haya. Kwa sababu inatambua kali za uhamisho, IFC PS 5 inasisitiza kuwa uhamisho wa lazima uepukwe. Pale ambapo uhamisho wa lazima hauwezi kuepukika, basi unapaswa kupunguzwa na hatua zinazofaa za kutuliza makali yake lazima ziandaliwe na kutekelezwa kwa uangalifu. Hii inapaswa kufanyika kwa mashauriano yenye maana na wale wanaoathirika. Masharti haya yanatumika hata kama uhamishaji unasimamiwa na serikali. Ikiwa hatua za uhamishaji wa serikali hazitimizi masharti ya PS5, Mpango wa Ziada wa Uhamishaji lazima uandaliwe ili kufidia mapengo hayo.

ESIA ya 2016 haielezi kikamilifu madhara ya mradi huo. Inaonyesha kwamba Mpango wa Utekelezaji wa Uhamisho utalenga jamii za wakulima huku ukipuuza jamii zingine ambazo zitahamishwa kiuchumi. Pia ESIA imeweka kiwango cha uhamisho kuwa kidogo kuliko kilivyo, huku ikieleza kwamba patahitajika ekari 880 za ardhi, wakati nyaraka zingine zinaonyesha kwamba angalau ekari 975 zitatumika kwa mradi huu. Zaidi ya hayo, ESIA haitoi maelezo zaidi juu ya idadi ya watu ambao watahamishwa, wala vigezo vya ustahiki au mbinu za fidia.

Kwa kawaida, kutengenezwa kwa Mpango wa Kurejesha Riziki (Livelihood Restoration Plan – RAP) kunaweza kuondoa udhaifu huu. Hata hivyo, sio wakati huu. Kutokana na ufahamu wetu, hakuna RAP au Mpango wa Kurejesha Riziki uliochapishwa au kushirikisha watu walioathirika. Badala yake, muhtasari wa RAP unapatikana mtandaoni. Muhtasari wa RAP ni muhimu zaidi kuliko ESIA 2016, lakini bado hauna maelezo muhimu:

- Haufafanui vigezo vya kustahiki kwa makundi mbalimbali ya watu waliohamishwa na mradi huo. Bado haijulikani vile watakatendewa wakulima ambao hawana hati miliki, lakini kwa kawaida wameitumia ardhi kwa mazoea ya kidesturi katika kiwanja cha makaa ya mawe. Hatma ya wakulima wa Kwasasi ambao wamehamishwa na barabara ya kufikia kiwanja bado haijulikani. Athari ya kutokuwa na uhakika huu ni kali.
- Haitambui kuwa baadhi ya watu walioathirika waliishi kwa msimu kwenye ardhi katika makazi za muda.
- Uhamishaji wa wavuvi umewekwa katika kiwango cha chini kuliko ilivyo. Inasema kuwa uhamisho hauzidi "3BMUs" (vitengo vya usimamizi wa pwani), ambao ni jumla ya wavuvi 124. Haitoi ramani au hoja ili kuunga mkono takwimu hii. Tunaamini kuwa inapunguza idadi ya wavuvi ambao wataathirika. Uvuvi unachukua nafasi ya pili katika mkubwa wa uchumi wa Lamu, baada ya utalii. Tunakadiria kwamba angalau wavuvi 4,700 wataathirika moja kwa moja na kiwanda cha makaa. (hii ni sawia na idadi ilinakiliwa kama waathiriwa na Makamaa makuu ya Kenya, katika kesi kuhusu bandari ya Lamu na LAPSSSET kwa ujumla). Wavuvi hawa hutumia maji ndani na karibu na Manda na wataathirika kutokana na kuzorota kwa mazingira ya baharini na vikwazo vya uvuvi na upatikanaji wa njia za meli.
- Haitambui athari mbaya za riziki kwa watu waoanofanya kazi katika sekta ya utalii. Utalii ndio unaochangia pakubwa katika uchumi wa Lamu. Wanaofanya kazi katika sekta ya utalii wanakabiliwa na athari kubwa katika maisha yao kwa sababu ya mabadiliko makubwa kwa utamaduni na mazingira ya Lamu.
- Haitambui kikamilifu madhara ambayo watapata watu wa asilia na jamii zingine zilizohatarishwa, kama ilivyojadiliwa katika kifungu kidogo cha F hapo chini: WaOrma, WaSanye, WaGiriama na Waswahili hawatambuliwi kabisa. Hakuna ithibati

ya kibali kuwa jamii asilia zimeipa FPIC matumizi ya ardhi ya kitamaduni ambayo wanaitumia wao.

Aidha, ESIA 2016 na muhtasari wa RAP hazionyeshi kuwa watu waliohamishwa watapata aina na ubora wa faida za uhamisho zinazohitajika na sera ya IFC. Muhtasari wa RAP unalenga fidia, ya fedha, hasara maalum (hesabu iliyotumiwa haiko bayana) na hauzingatii mambo muhimu katika kurejesha riziki. Mpango wa RAP au Urejesho wa Riziki, unaohitajika na IFC PS 5, unapaswa kutimiza hali zote mbili. Kwa mfano:

- Muhtasari wa RAP unasema kwamba wachuuzi wa mikoko watalipwa fidia kwa kupoteza riziki kwa muda wa mwaka mmoja wakati wanapojifahamisha na vyanzo vingine vya mapato, bila kuahidi msaada wowote au kuungwa mkono ili kujiruzuku.
- Vilevile, muhtasari wa RAP unasema kwamba wavuvi ambao watapoteza misingi yao ya uvuvi watafidiwa kwa mwaka mmoja kwa kupoteza riziki. Pia watapewa vyombo vya kisasa vya uvuvi na dau ili kuwawezesha kuvua mbali na pwani. Waraka huo hauna uchambuzi wa kina wa jinsi gani wavuvi watahamasishwa na kusaidiwa kuanza uvuvi wa mbali na pwani, na kama fidia ya mwaka mmoja itatosha.
- Kwa watu wa Aweer (watumiaji wa jadi eneo linalokusudiwa mradi), muhtasari wa RAP unasema kwamba "watazingatiwa ili kupata zisizohitaji na ujuzi katika mradi wa kiwanda wakati wa awamu ya ujenzi na uendeshaji." Jibu jili halifai kabisa kwa jamii za asilia ambazo zinakabiliwa na vitisho mbalimbali dhidi ya urithi wao wa kitamaduni, pamoja na athari za riziki kutokana na mradi.

Kutokana na uhaba wa taarifa kuhusiana na athari za uhamishaji na mipango ya kutuliza makali, pamoja na upungufu wa nyaraka zilizopo, maendeleo yoyote katika kiwanda cha makaa yataavunja masharti ya IFC PS 5.

F. Tathmini zinapuuzwa watu asilia

Katika IFC PS, kuna kanuni za kutambua na kuzingatia maslahi maalumu ya watu asilia. Pia, IFC PS 7 (watu asilia) inawajibisha wanatekelezaji wa mradi unaoathiri jamii asilia, ikiwa ni pamoja na:

- Kanuni za kutekeleza mchakato wa Ushauriano na Ushiriki wenye Ufahamu (ICP) unaojumuisha mashirika ya jamii asilia pamoja na wanajamii wenyewe.
- Kanuni za kuepuka na kupunguza kiasi cha ardhi iliyopendekezwa kwa mradi huo na athari nyingine mbaya kwenye maliasili.
- Kanuni za ziada za uhamishaji, ikiwa ni pamoja na mahitaji ya kuunda Mpango wa Watu Asilia (IPP), kutoa fidia inayofaa kitamaduni na fursa endelevu za maendeleo, na, kukiwa na kuhamishwa au athari mbaya juu ya turathi za kitamaduni muhimu, kufuata kanuni za Mwafaka Huru, wa Awali na wenye Ufahamu (FPIC).

Kaunti ya Lamu ina jamii asilia ambazo ni pamoja na Wabajuni, Waswahili, Wasanye, Waaweer (pia wanajulikana kama Waboni), na Waorma, vile vile WaGiriama, WaMijikenda, WaMaasai wa Kore na wengineo. Wabajuni wataathiriwa zaidi kwa kupoteza maeneo ya jadi ya uvuvi na mikoko. Makundi yote pia yatapoteza maeneo ya lishe kwa mifugo, uwindaji, na uokotaji na uvuvi ndani na katika eneo la mradi na yatapata athari kwa turathi za kitamaduni. Athari kutokana na kiwanda cha makaa yataongezea kwa hasara zilizopo kwa sababu ya maendeleo ya bandari ya Lamu.

Eneo la jadi la Waaweer liko kaskazini mashariki ya Kaunti ya Lamu, ikiwa ni pamoja na mazingira ya Misitu ya Boni na Dodori. "Eneo hili limekuwa makazi yetu tangu jadi ... Pia tunazingatia misitu sana kwa kuwa tuna maeneo mengi matakatifu yaliyohifadhiwa humo

ndani." Watateseka Zaidi kutokana na ukataji miti na kuhamishwa kutoka kwa sehemu za jadi uwindaji na kukusanya.

Waorma ni nusu wachungaji na wahamaji, ambao huhamisha ng'ombe wao kote katika bara ya Lamu kutafuta malisho mazuri. "Tunatambua maeneo ya misitu na majani katika sehemu ya magharibi ya Kaunti kama ardhi ya ufugaji wa jadi. Kutoka Witu, tunahamia kaskazini kuelekea maeneo ya misitu hadi nyanda za Mto Tana."

Wabajuni pia wana "maeneo ya kilimo cha kijamii katika bara na hupanda mahindi, ufuta na mtama, pamoja ya mazao mengine."

Wasanye hutumia misitu kukusanya asali, matunda, na mizizi. Wao pia ni wakulima wadogo wadogo. Kijadi, waliishi katika misitu ya kusini na ukanda wa mbuga za Lamu kati ya Kisiwa cha Lamu na mji wa Witu, barani. Hata hivyo, wamekuwa wakiondolewa kwa nguvu na miradi ya serikali ya uhamishaji, wakiwachwa kutawanyika katika maeneo ya mijini na vijiji vidogo bila usalama wa ardhi.

Waswahili pia ni wakulima, wavuvi na wafugaji, pamoja na wafanyabiashara wa bidhaa za kilimo zinazozalishwa na makundi mengine.

"Katika jumuiya yetu huko Lamu, tuna makundi kadhaa ya riziki ambayo yanaunganishwa na kuingiliana. Makundi ya kikabila ndani ya Lamu mara nyingi hushirikiana katika riziki - na kwa sababu hiyo, jamii zinaishi kwa amani kwa sababu zinaingiliana ili kujiruzuku."

Upotevu wa riziki utakuwa na athari za kiuchumi, maarifa ya jadi na turathi za kitamaduni. Endapo hazifanyishwi kazi, mbinu za jadi huotea

"Kilimo ni riziki yetu – na pia tuna mila na desturi za kitamaduni na kiroho zinazojumuishwa na kilimo chetu."

Jamii hizi pia zinaogopa kupoteza uwezo wa kufikia maeneo muhimu ya kitamaduni. WaSanye "tayari wamepoteza makaburi yao na tuna hofu kubwa kwamba tutaendelea kupoteza maeneo zaidi."

Hatimaye makundi yanaogopa madhara yanayohusiana na uhamiaji wa watu, ikiwa ni pamoja na uharibifu wa mazingira, uharibifu wa maadili na utamaduni, na kutengwa zaidi katika jamii.

ESIA 2016 na Muhtasari wa RAP hazitambui vyema jamii hisi asilia. Hakuna ithibati kwamba ushauriano wa maana, bila hata FPIC, umefanyika na jamii hizi. Wakati jamii za Waaweer na Wabajuni zimeelezwa kwa ufupi katika ESIA na Muhtasari wa RAP, hakuna hatua za kutosha zilizowekwa ili kuwalinda kutokana na madhara mabaya ya mradi huu. Kuhatarishwa na kutengwa kwa watu asilia kunazidishwa na namna wanavyopuuzwa na waendelezaji wa mradi.

G. Turathi za kitamaduni zinatishwa

Mbali na vitisho maalumu vinavyowakabili watu asilia, jamii ya Lamu inakabiliwa na athari mbaya juu ya turathi zake za kitamaduni zenye thamani kubwa Tunaafikiana na maoni yaliyolewa na UNESCO kuhusu athari za LAPSSSET na kiwanda cha makaa juu ya turathi za kitamaduni. Kuhusu hasa kiwanda cha makaa, UNESCO inataja hatari zifuatazo:

- Kupoteza mila na desturi zinazohusiana na riziki zitokanazo na uvuvi;
- Tishio kwa majengo ya mawe maridadi katika Lamu Old Town na mahali kwingine kutokana na uchafuzi wa hewa;

- Athari za ongezeko la watu (ikiwa ni pamoja na maendelo yasoyodhibitiwa, ukosefu wa usalama, hali ya afya) na mabadiliko ya tabia za Uswahili za jamii hiyo; na
- Athari za ujumi kutokana na miundombinu ya kiwanda cha makaa.

UNESCO inasema kuwa ESIA ya 2016 haishughulikii hatari hizi. ESIA ya 2016 inapendekeza mfululizo wa sheria na kanuni juu ya wafanyakazi wake na makandarasi, kwa mfano kutoa taarifa "pato za bahati" na kuvaa kwa kiasi kizuri. Hata hivyo, kanuni hizi hazipo sawa na athari kubwa juu turathi za kitamaduni zitakazotokana na na mradi huo. ESIA ya 2016 inashindwa kushughulikia maswali muhimu zaidi kama makazi ya wafanyakazi na idadi ya watu na aina ya wafanyakazi (ikiwa ni pamoja na umri na ukabila). Kama UNESCO inavyosema, "[ESIA] haiweki mizani ifaayo kuhusu madhara ya idadi ya watu na mabadiliko ya tabia za Uswahili ... Ni maisha ya kila siku ya kijamii na ya kitamaduni yatakayoathiriwa sana, na suala hili linahitaji kuchunguzwa na kueleweka vyema kabla ya hatua za kupunguza makali ya madhara kutengenezwa."

ESIA ya 2016 pia haijagusia uwezo wa athari kwa maeneo ya jadi ikiwemo misikiti miwili na makaburi na visima ambazo zinaweza kuathiriwa na mjengo huu. Aina hizi sa maneno ni alama na njia za kutunza mila na desturi za jamii na pia utambulisho.

Tathmini hii ya juu juu na isiyokuwa na kina ya turathi za kitamaduni inakiuka kanuni za IFC PS 1 na 8 (turathi za kitamaduni). Utamaduni maalumu, wa kihafidhina na uliohifadhiwa na Lamu Old Town na mazingira yake, kama maeneo ya turathi ya kitamaduni inayotambulika kimataifa, ni "turathi muhimu ya kitamaduni" kwa minajili ya IFC PS 8. Kwa hivyo, mradi huo lazima uepoke madhara kwa "turathi hii muhimu ya kitamaduni." Katika mazingira ya kipekee ambapo madhara hayawezi kuepukika, mradi lazima uonyeshe matokeo yatakayopatikana na mchakato mzuri wa kujadiliana na jamii zilizoathirika. Wataalamu wa nje wanapaswa kubakia ili kusaidia katika tathmini na ulinzi turathi muhimu wa kitamaduni. ESIA 2016 haitoi ushahidi kwamba mahitaji hayo yametimizwa.

H. Tathmini Mbadala inategemea dhana potovu na mantiki isiyofaa

Kama ilivyojadiliwa kwa kirefu katika malalamishi, inajulikana wazi kuwa viwanda wa makaa ni hatari kwa afya ya binadamu na hatari zinazohusiana na hali ya hewa. Kwa hivyo, World Bank Group itatoa msaada wa kifedha tu kwa miradi ya makaa kijani katika hali chache pekee. IFC PS pia inapaswa kutafuta njia mbadala kwa ajili ya mradi na muundo wake, ili kujiepusha na athari mbaya za kimazingira na kijamii. Uchunguzi mbadala uliofanywa kwa ajili ya kiwanda cha makaa hauwezi kufikia viwango hivi muhimu:

1. ESIA haina mantiki ya kutosha kwa kukataa vyanzo vya nishati safi

Tathmini mbadala ya kiwanda cha makaa imetegemea hoja zisizofaa ili kukataa vyanzo vya nishati visivyochafua mazingira. Kwa mfano, ESIA inasema kuwa nguvu za jua na nguvu za upepo haziwezi kuhifadhiwa au kutumika kama vyanzo vya msingi. Inasema tena kuwa hakuna aina nguvu inayopaswa kuongeza asilimia 10% ya wastani wa mahitaji ya umeme," la sivyo, gridi haitakuwa thabiti." Madai hayo si ya kwei, kama iliyoelezwa katika utafiti wa karibuni uliochapishwa na wanasayansi wa Chuo Kikuu cha Stanford.

2. Tathmini mbadala haitoi sababu za kutosha za kuchagua eneo la mradi

Tathmini ya ziada ya maeneo mbadala inazingatia tu gharama na inapuuza masuala ya kijamii na mazingira. Kwa mfano, haitoi fursa ya kuchagua maeneo ya bara ambayo inaweza kupunguza athari za mazingira ya pwani, pamoja na shinikizo la Lamu Old Town, kwa sentensi mbili tu, ikitaja gharama kubwa bila kuzingatia mambo mengine. Jambo hili ni kinyume kabisa

na kanuni za IFC PS zinazoagiza wanamradi kujiepusha na kuhamisha watu na athari kwa mazingira muhimu na makazi ya asili ya viumbe kadri iwezekanavyo.

3. *ESIA haitathmini njia mbadala ambavyo ni safi kwa vipengele muhimu vya usanifu*

ESIA ya 2016 pia inashindwa kuchunguza vizuri vipengele vya usanifu ambavyo ni safi, ikiwemo mbinu ya kuchemsha, mfumo wa kuweka baridi na kutunza kwa jivu. Kwa mfano, uamuzi wa kutumia mfumo wa kuweka baridi moja kwa moja umeelezwa katika sentensi moja tu, ikisema kuwa hili ni chaguo bora zaidi kwa ajili ya baridi, bila kutambua hatari zake kubwa zaidi kwa mazingira ya baharini. Ripoti haitathmini kwa kina njia mbadala za kimazingira kama vile utiaji baridi kwa unyevunyevu mzunguko. Tathmini hi indigo haitoshi na haiwezi kudhihirisha manufaa ya kimazingira na kijamii kwa usanifu mbadala.

I. Athari za kijumla za LAPSSET zimepuuzwa

Mbali na athari za moja kwa moja za mradi huu, IFC na wateja wake wanatakiwa kuzingatia "Athari kijumla ambazo hutokea ... kutokana na maendeleo mengine yaliyomo, yaliyopangwa au yanayofafanuliwa."

Tathmini ya athari ya ESIA ya 2016 ya kijumla iitwayo 'Cumulative Impact Assessment (CIA)' inatambua kuwa miradi kadhaa "inatarajiwa" katika eneo hilo, ikiwa ni pamoja na vipengele vya mradi wa LAPSSET. Hata hivyo, miradi hii haijumuishwi katika CIA kwa sababu inadai kwamba wakati wa utekelezaji wake haujulikani.

Kupuuzwa huku sio halali. Vipengele vya mradi wa LAPSSET vinavyohusika na Kaunti ya Lamu sasa viko katika hatua mbalimbali za maendeleo, na baadhi ya vipengele hivyo viko katika maandalizi ya mapema wakati vingine vinajengwa. Kuvunjwa ardhi ili kuanza Bandari ya Lamu kulifanyika mwaka 2012, na tangu wakati huo, vituo mbalimbali vya miundombinu vimejengwa. Uboreshaji wa uwanja wa ndege wa Manda tayari umekamilika, tangu mwanzo mwaka 2011. Vipengele vingine vya LAPSSET vilikuwa vimepiga hatua kubwa za upangaji wakati Ripoti ya ESIA ikichapishwa.

Kila sehemu ya LAPSSET ina hatari na athari za kipekee, tangu athari za mazingira zinazohusiana na kazi nyingi za ujenzi katika mji mdogo hadi athari nyingi za kijamii ambazo zitaambatana na ongezeko kubwa la idadi ya watu. Kwa pamoja, miradi hii ina uwezekano wa kuwa na madhara makubwa kwa watu na mazingira katika Kaunti ya Lamu. Hii ndiyo hali ambayo kanuni za CIA ya IFC zilitarajiwa kushughulikia.

J. Watu walioathirika hawatapa manufaa ya mradi - na hili litasababisha wanajamii kutounga mkono

IFC PS inatambua kuwa uungwaji mkono na wanajamii na ugawaji wa manufaa ni muhimu sana ili kuwa na usimamizi wa kina na kupunguza hatari za kimazingira na kijamii. IFC inatarajiwa kuchunguza kama wanajamii wanaunga mkono mradi katika hali ambapo kuna athari kubwa kwa wanajamii. IFC PS pia hutarajia kuwa jamii zilizoathirika zinapata manufaa kutokana na mradi: hali ambayo ni ya lazima endapo uungwaji mkono utapatikana.

Amu Power imefanya jitihada ndogo sana ili kuhakikisha kwamba jamii zinazoathirika na mradi huu zitapata manufaa ya msingi ya mradi: umeme. Amu Power haijawahakikishia wakazi wa Lamu kwamba watapata umeme. Fauka ya hayo, tunaelewa manufaa ya ajira kutokana na mradi imetiwa chumvi, kwa sababu asilimia arobaini (40%) ya kazi zote itaenda kwa Wachina.

IV: Juhudi za kuwasilisha masuala haya kwa Amu Power, wawekezaji na mamlaka zingine

Wajumbe wa Save Lamu na Kwasasi Mvunjeni Farmers Self-Help Group wamehudhuria mikutano ya mashauriano ya wadau ili kutaja matatizo haya. Maswali yetu hayakujibiwa au yalijibiwa kwa kupuuzwa, na habari za kupotosha. Wajumbe wa Save Lamu pia wamejaribu kushiriki katika mikutano ya ziada lakini wamekuwa kutengwa na kufanywa kutojisikia salama. Isitoshe, tumetoa maoni kwa njia ya maandishi, moja kwa moja kwa Amu Power, wanahisa wake (Gulf Energy na Centum), wawekezaji wake (ikiwa ni pamoja na IFC) na mamlaka za serikali zinazohusika, na kwa njia ya moja kwa moja ya taratibu rasmi za kushauriana. Kwasasi Mvunjeni Farmers Self Help Group wameweka malalamishi yao wazi (bila mafanikio) na pia wametuma barua za kupewa maelezo zaidi kwa Serikali.

Licha ya majaribio haya mazuri ya imani ya kushauriano, hatujawahi kupokea ushirikiano wa kina kuhusu hofu zetu.

Kwa hivyo, malalamishi haya yanataka ofisi ya CAO ifanye tathmini ya ridhaa na kuchunguza IFC na ridhaa ya wateja wake ili kujua kama wamefuata kanuni za mazingiza na kijamii, viwango, na masharti. Tunatarajia kuwa CAO itapata ushahidi wa kutosha na *usiopingika* wa kukiukwa kwa viwango hivyo.

Kwa hiyo, IFC inapaswa kuchukua hatua za haraka ili kuzuia wateja wake kushiriki katika mradi huu hatari na ikague uwekezaji mpya katika Sekta ya kifedha ya Kenya kwa makini ili kuepukana na mchango wowote zaidi wenye madhara.